WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

CHUO CHA UALIMU MPWAPWA

KANUNI ZA CHUO

Kila mwanachuo anatakiwa awe na mwenendo mzuri unaolingana na kazi ya Ualimu pia na lengo la Taifa kuhusu falsafa ya Elimu ya kujitegemea. Imani ya Taifa letu iwe ndiyo msingi wa mwenendo, fikra na tabia njema. Kila mwanachuo lazima asome, aelewe na akubali masharti yote yaliyomo katika mkataba atakaouwekea sahihi kati yake na serikali (In-service and Pre-service Training Agreement). Kila Mwanachuo atalazimika kufuata miongozo mbalimbali inayotolewa chuoni mara kwa mara.

1. **(A) RATIBA**

Kila Mwanachuo lazima ahudhurie vipindi vilivyomo kwenye ratiba ya kila siku. Mwanachuo anapaswa kuamka saa 11:15 alfajiri na kulala saa 5: 30 usiku. Ratiba hiyo inaonesha shughuli zote za nje na ndani ya darasa. Ni lazima kila mmoja awahi kufika katika kila shughuli atakayopangiwa, na afanye kazi kwa bidii na juhudi bila kusimamiwa.

(B) MATUMIZI YA SIMU

Mwanachuo haruhusiwi kutumia simu kwa namna yoyote ile wakati wa vipindi darasani **isipokuwa** kwa ruhusa maalumu ya Mkufunzi. Ukiukwaji wa kanuni hii utamfanya mtumiaji wa simu kunyang'anywa simu yake na kutunzwa/ kushikiliwa na Mkufunzi/Ofisi mpaka mwisho wa muhula. **Mwanachuo atakayegoma kutoa simu atalazimika kurudishwa nyumbani.**

(C) DARASANI

i. Kila mwanachuo anatakiwa kuwa msikivu katika vipindi na kusoma kwa makini wakati wote anapokuwa darasani. **Kila Mkufunzi wa somo ataweka kumbukumbu ya mahudhurio ya wanachuo wa somo lake, hivyo kushindwa kuhudhuria darasani kwa kila somo bila ruhusa, ni utoro na utalazimika kurudishwa nyumbani.**

ii. Wakati wa kipindi cha kujisomea usiku, mwanachuo atatakiwa kuwa darasani au maktaba tu.

iii. Kila mwanachuo anatakiwa kuhudhuria masomo darasani au nje ya darasa. Mahudhurio yasiwe chini ya siku 194 kwa mwaka au siku 97 ndani ya mhula mmoja au 75% ya vipindi vyote ambavyo kila mwanachuo anatakiwa kuhudhuria kulingana na mpango wa mafunzo husika. **Kutotimiza siku au asilimia hizo kutamfanya mwanachuo kupoteza sifa ya kufanya mitihani ya muhula hivyo kulazimika kurudia mwaka**.

iv. Ni LAZIMA kila mwanachuo kuhudhuria na kufanya mitihani, majaribio na mazoezi yatakayotolewa na mwalimu wa somo, idara au chuo, ukikiuka kanuni hii unakosa sifa ya kuendelea na mafunzo.

(D) UTARATIBU WA KUBAKI CHUONI

(i) Ikiwa italazimika kubakiza baadhi ya Wanachuo chuoni, ni wajibu wa kila mwanachuo kubaki chuoni kwa utaratibu utakaowekwa na chuo kwa ajili ya kutunza mali/miradi ya chuo. Hii ni sehemu ya wajibu wa kila mwanachuo ikiwa ni pamoja na kufuata kanuni na taratibu zote za chuo.

(E) KUSANYIKO MAALUMU (ROLL CALL)

Kila mwanachuo ni lazima ahudhurie Kusanyiko maalumu (Rollcall) kila Jumamosi, Jumapili na siku za sikukuu saa 10:30 jioni. Kengele itagongwa saa 10:15 na ifikapo saa 10:30 maelekezo yatatolewa, na kwa yeyote atakayefika baada ya saa 10:30 atahesabiwa mtoro na adhabu kali itatolewa.

(F) WAGONJWA

(i) BIMA: Kila mwanachuo atatakiwa kuchangia gharama ya matibabu kama ilivyoelezwa kwenye barua ya maelekezo ya kujiunga na chuo ili kupata bima ya Taifa (NHIF).

(ii) Wagonjwa wote watatakiwa kwenda kumwona mganga katika zahanati ya chuo kuanzia saa 1:30 Asubuhi baada ya kuandika jina kwenye kwenye ofisi ya zamu. Mganga pekee ndiye atakayeruhusu mgonjwa aende hospitali kuu ya wilaya na kama anastahili kupumzika bwenini, atampa idhini ya kupumzika (Bed rest). Anayepewa idhini na Mganga aripoti kwa **Mkufunzi wa zamu** na ofisi ya mwadili ili idadi ya wote wenye ruhusa ya Daktari kwa siku hiyo ijulikane. Ikumbukwe kuwa kuwa na ruhusa(Bed rest) nyingi zinaweza kusababisha mwanachuo kuachishwa/kusimamishwa mafunzo kwani chuo kitamhesabu kuwa hayuko timamu kiafya (physically fit) kumudu kuendelea vema na mafunzo.

(G) MAZOEZI YA VIUNGO

Ni agizo la serikali kusisitiza ratiba ya mazoezi ya viungo vyuoni na shuleni, hivyo ni wajibu wa kila mwanachuo kuhudhuria mazoezi ya viungo siku ya Jumamosi saa 12.00 Alfajiri hadi saa 1.15 Asubuhi. Adhabu kali itatolewa Kwa mwanchuo yeyote atakayeshindwa kuhudhuria kipindi hicho cha mazoezi ya viungo ikiwa ni pamoja na kusimamishwa mafunzo kwa muda ambao kamati ya nidhamu itaona unafaa.

(H) DINI

Chuo kinatambua na kuheshimu uwepo wa imani za dini mbalimbali na chuo kinasistiza ushirikiano miongoni mwa waamini wa imani hizo. Hata hivyo shughuli zote za kidini zinatakiwa kufuata utaratibu uliowekwa kulingana na ratiba ya chuo.Vipindi vya dini jioni vitaanza saa 12:50 na kuisha saa 1:50 usiku.

2. USAFI

a) Mazingira

(i) Kila mwanachuo atatakiwa kutunza Mazingira ya chuo na katika eneo alilopewa kuhudumia

kufagia na kumwagilia maua. Hairuhusiwi kabisa kutupa taka eneo lisiloruhusiwa.

(ii) Kila mwanachuo atatakiwa kuhakikisha kuwa eneo la makazi (bwenini) na darasani ni safi wakati wote na maua kuzunguka viunga vya bwenini na darasani yamwagiliwe kila siku. Kushindwa kufanya hivyo kutaambatana na adhabu kali ikiwa ni pamoja na kutolewa darasani ili kufanya kazi hiyo au kurudishwa nyumbani kwa muda utakaoamuliwa na kamati ya nidhamu.

b) Usafi wa Mwili

Usafi wa mwili, nguo na mazingira ni dalili ya tabia njema na utu uzima. Kila mwanachuo daima anatakiwa kuweka mwili wake, nguo, na mazingira katika hali ya usafi.

(i) Wanachuo wa kiume hawaruhusiwi kabisa, kufuga kucha ndefu, ndevu, sharafa, sharubu, nywele ndefu kupita kiasi, denge au panki. Hakikisha kuwa ndevu na sharafa zinanyolewa wakati wote. Ni kosa kubwa kuvalia nguo chini ya kiuno (kata K), hatua kali zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kuachishwa mafunzo (kufukuzwa) kwa kosa hilo.

(ii) Wanachuo wa kike hawaruhusiwi kufuga kucha ndefu, kutumia rangi za kucha, kupaka wanja, rangi ya mdomo, kutumia madawa ya kuchubua ngozi, kubadili rangi ya nywele. Pia bangili, mikufu, shanga na hereni za kuning'inia na za kubana zaidi ya moja haviruhusiwi kuvaliwa. Kila mwanachuo atakaye suka nywele asuke mtindo wa kuzirudisha nyuma **(Utii wa roda**) na atakaye zibana azibane kwa kurudisha nyuma na kutumia kibanio cha rangi ya bluu bahari au nyeusi.

3. CHAKULA

(a) Milo yote iliwe ndani ya ukumbi wa chakula au eneo lililoandaliwa. **Ni marufuku kupeleka chakula bwenini**. Si vizuri mwanachuo kula akiwa amesimama. Wagonjwa walioruhusiwa na matron/patron au mganga wa Zahanati/Hospitali wanaweza kulia chakula bwenini/hospitali.

(b) Ni marufuku kupika aina yoyote ya chakula bwenini, na/kumiliki silaha bwenini kama kisu nk. Hatua kali zitachukuliwa dhidi ya mwanachuo yeyote atakayekiuka kanuni hii, ikiwa ni pamoja na kufukuzwa chuo.

(c) Wanachuo wote watakula chakula kilichotolewa na chuo kwa wote, chuo hakina chakula maalum (Special diet)

(d) Kila mwanachuo lazima azingatie kikamilifu saa za chakula na taratibu za kupewa/kugawiwa chakula. Anayechelewa kufika kwenye ukumbi wa chakula au asiyetaka utaratibuwa wa kugawiwa chakula bila sababu maalumu hastahili kupewa chakula. Kukiuka kanuni hii ni utovu wa nidhamu na ukosefu wa ustaarabu. Adhabu kali itatolewa kwa kosa hili.

(e) Si vizuri kupiga kelele, kumwaga ovyo chakula mezani au kuviacha vyombo vya chakula pamoja na Ukumbi katika hali ya uchafu. **Usafi ni dalili ya uungwana.**

(f) Ili kuepuka magonjwa ya mlipuko, Huruhusiwi kununua chakula cha aina yoyote barabarani au katika eneo linalozunguka chuo. Vyakula vinunuliwe kwenye idara ya sayansi kimu, mgahawa wa chuo au kwa wakala aliyeruhusiwa na chuo.

4. NIDHAMU

Ni muhimu sana kudumisha uhusianao mwema kati ya wanachuo na jumuiya yote ya chuo na jirani zetu, ili jina lako na jina la chuo lijengwe kutokana na busara na vitendo vyako kwa hiyo:

i. Kila mwanachuo atatakiwa kuonesha heshima kwa viongozi wake, wakufunzi, wafanyakazi wote, wanajumuiya wote nje na ndani ya chuo. Ni wajibu wa kila mwanachuo kumsalimu kiongozi akiwa amesimama.

ii. Kila mwanachuo anatakiwa kutumia kwa busara sana lugha na vitendo vyake wakati wote nje na ndani ya chuo. Kila mwanachuo anawajibika kuwa mfano mzuri kwa matendo na tabia njema mahala popote.

iii. Ugomvi, kupiga, kupigana, majungu, uchochezi, sherehe na vikao visivyo rasmi, vikao vya kikabila, Ukanda au uzawa ni marufuku kabisa kwa mwanachuo/ wanachuo.

iv. Kusema Uongo ni dalili ya utovu wa nidhamu. Hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya mwanachuo atakayeonekana na tabia hiyo.

v. Wizi wa kitu chochote ni kosa kubwa sana na adhabu yake ni kufukuzwa kabisa chuoni. Mwizi anaweza kufunguliwa mashtaka mahakamani kwa kosa la jinai.

vi. Ni kosa kubwa kutoroka kwenda nje ya eneo la chuo / nje ya Mpwapwa. Hatua kali zitachukuliwa kwa kosa hili ikiwa ni pamoja na kufukuzwa chuo.

vii. Mwizi, mgomvi, mtovu wa adabu anaweza kufukuzwa chuoni, bila kujali kuwa kosa lake litakuwa limefikishwa mahakamani au hata kama ameshinda kesi.

viii. Mwanachuo yeyote hataruhusiwa kuendelea na mfunzo akigundulika kuwa ana mimba au amempa mimba mwanachuo mwenzake au mwanafunzi yeyote.

5. AFYA YA UZAZI

a) Chuo hakina mahali / namna ya kutunza wajawazito. Hivyo mwanachuo yeyote atakayebainika kuwa mjamzito **atasimamishwa mafunzo** yake ili apate muda wa kulea mimba na baadaye mtoto tarajali angalau kwa muda usiopungua miaka mitatu kabla ya kuomba upya kuanza masomo.

b) Wanachuo wa kike watatakiwa kupima afya zao (Ujauzito) kwenye kituo cha afya au hospitali kabla au baada ya usajili na wakati mwingine wowote itakapolazimu kufanya hivyo, atakaye bainika kuwa ni mjamzito atatakiwa kusimamishwa mafunzo.

c) Kujaribu kutoa au kutoa mimba ni kosa la jinai. Mwanachuo yeyote atakayebainika kutenda kosa hilo atafukuzwa chuo na anaweza kushitakiwa kwa mujibu wa sheria za nchi ikilazimu kufanya hivyo.

d) Ili kuepukana na uambukizaji / uambukizwaji wa magonjwa ya zinaa hasa UKIMWI (AIDS) ni **marufuku kujihusisha na mapenzi, ufuska na uasherati nje na ndani ya chuo. Ukiukaji wa kanuni hii ni kufukuzwa kabisa chuoni.**

e) Mwanachuo yeyote atakayebainika kujihusisha na mapenzi, ufuska na uasherati kwa wanafunzi wa shule wakati wa mazoezi ya kufundisha kwa vitendo (BTP) na ushahidi ukabainika, mwanachuo/wanachuo huyo/hao watafukuzwa kabisa chuoni. Aidha mwanachuo akionesha utovu wa nidhamu wowote ambao tutaubaini au kuripotiwa na uongozi wa shule, hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa.

6. **MARUFUKU:**

i. Ni marufuku kwa mwanachuo yeyote kushawishi, kujihusisha au kushiriki mgomo wa aina yoyote.Ukiukaji wa kanuni hii, adhabu yake ni kufukuzwa chuo

ii. Ni marufuku kuacha taa zinawaka mabwenini na madarasani au kuacha bomba la maji likitiririsha maji ovyo. Adhabu ya kosa hii itaamuliwa na kamati ya nidhamu.

iii. Ni marufuku kuhifadhi au kutumia silaha ya aina yoyote wakati wowote mwanachuo awapo chuoni au nje ya chuo .Ukiukaji wa kanuni hii ni kufukuzwa chuo.

iv. Ulevi ni kosa la kinidhamu na kiutumishi, ni marufuku Mwalimu tarajali/Kazini kulewa, kuingia vilabu vya pombe, nyumba za pombe, nyumba za wageni (Guest Houses) ukiwa chuoni na sehemu za makahaba. Ukiukaji wa kanuni hii ni kufukuzwa chuo.

v. Ni marufuku kwa wasichana kuingia mabweni ya wanaume au wanaume kuingia mabweni ya wasichana bila ruhusa ya Mwadili au mkufunzi.

vi. Ni marufuku kwa mwanachuo yeyote kuingia nyumba ya Mkufunzi, Mfanyakazi wa chuo na za watu wengine na maeneo yake isipokuwa kwa kibali cha maandishi toka kwa Mwadili. Adhabu kali itatolewa na mlezi/kamati ya nidhamu kwa kukiuka kanuni hii.

vii. Ni marufuku kuuza, kuweka au kutumia aina yoyote ya **Kilevi** bwenini, darasani, ukumbi wa chakula/ mahali pengine popote chuoni. Pia ni marufuku kutumia au kuhifadhi madawa ya kulevya. Adhabu ya kosa hili ni kufukuzwa chuo.

viii. Ni marufuku kuvuta sigara ndani ya eneo la chuo ikiwemo madarasani, maktaba, kwenye ukumbi wa chakula. Ukumbi wa chuo au mbele ya wafanyakazi/walezi. Kamati ya nidhamu itatoa adhabu kali kwa kosa hili.

ix. Ni marufuku kwa mwanachuo yeyote kujiunganishia umeme kwa madhumuni yoyote yale ikiwa ni pamoja na kuchemsha maji, kupigia pasi, kutumia kwenye redio, TV, na bedswitch. Hatua kali zitachukuliwa dhidi ya mwanachuo / wanachuo watakao husika ikiwa ni pamoja na kulipa gharama na kunyang'anywa vifaa vinavyohusika na kuviteketeza au kufukuzwa chuo.

x. Ni marufuku kuchora /kuandika au kubandika matangazo kwenye kuta za majengo yote ya chuo, kubandika picha, kugonga misumari na kuhamisha kifaa chochote cha chuo toka eneo moja kwenda eneo jingine bila kibali cha maandishi. Adhabu ya kosa hili ni kutengeneza sehemu iliyoharibiwa kwa fedha ya aliyeharibu, na kupewa adhabu nyingine ikiwa ni pamoja na kufukuzwa chuo. Matangazo yabandikwe sehemu zilizoruhusiwa.

xi. Ni marufuku kwa mwanachuo **kukataa kufungua mlango atakapotakiwa kufanya hinyo** aidha na kiongozi au Mkufunzi ikiwa atabainika au kutuhumiwa kwa kosa lolote la kinidhamu. Adhabu ya kosa hili ni kufukuzwa chuo.

xii. Ni marufuku kwa mwanachuo kupeleka mashitaka yoyote nje ya chuo (Polisi ,nk) bila kupata kibali cha Mwadili (Mlezi wa Wanachuo). Mashitaka yote yatashughulikiwa chuoni.

MUHIMU: Adhabu ya mwanachuo atakaye tenda kosa lolote la marufuku ni kufukuzwa chuo

7. RUHUSA:

(i) Kila mwanachuo anaruhusiwa **kutoka nje ya eneo la chuo akiwa katika sare** kama utaratibu wa jumapili na siku za sikukuu unavyoelekeza.

(ii) Kwa shida maalumu siku nyingine yoyote, ruhusa itatolewa na Mwadili / Mkufunzi wa zamu kwa maandishi / cheti cha ruhusa.

(iii) Ruhusa ya kutoka nje ya chuo kwa zaidi ya siku moja itatolewa naMwadili au Mkuu wa chuo. Kuchelewa kurudi zaidi ya muda ulioruhusiwa bila taarifa / kibali ni kosa kubwa na hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kufukuzwa chuo.

(iv) Ruhusa ya kuacha Mafunzo na kuingia mafunzo mengine nje ya Ualimu hutolewa na Mkurugenzi wa mafunzo ya Ualimu baada ya Mkuu wa chuo kuridhika Uamuzi huo.

(v) Hairuhusiwi kutoka nje ya chuo baada ya saa 11:30 jioni bila ruhusa ya mkufunzi wa zamu au Mwadili.

8. WAGENI:

(i) Siku za wageni kuwatembelea wanachuo ni Jumapili na siku za sikukuu na mwisho ni saa 10:30 jioni. Siku za Jumapili na siku za sikukuu wageni watapaswa kutoa taarifa kwa Mwadili wa Wanachuo au Mkufunzi wa zamu. Ni marufuku kumpeleka mgeni bwenini. Wageni wakaribishwe kwenye ukumbi wa starehe chuoni au ofisi ya zamu.

(ii) Kwa siku za masomo, wageni wote wanaotaka kuwaona wanachuo watapata kibali toka kwa wakufunzi wa zamu au Mwadili wa wanachuo.

2022-2023

9. BARUA NA MAKALA:

(i) Barua zote za kiofisi, taarifa na makala yoyote inayohusu masuala ya chuo inayopelekwa kwenye gazeti, redio na mitandao yote ya kijamii hapa nchini au nchi za nje, ni lazima vipitie kwa Mkuu wa chuo kupata idhini ya kutoa taarifa hiyo. Kutotii utaratibu huu ni kosa kubwa na adhabu yake itaamuliwa na kamati ya nidhamu kulingana na aina ya Taarifa.

(ii) Mawasiliano yoyote yanayohusu chuo na mtu, kampuni binfsi au umma lazima yapate kibali kutoka kwa Mkuu wa chuo. Mwanachuo atakayetenda kosa hili atasimamishwa mafunzo.

10. ULINZI NA USALAMA WA MALI YA UMMA

i. Ni wajibu wa kila mwanachuo kuhakikisha kuwa vifaa vyote alivyokabidhiwa au vilivyopo hapa chuoni vinahifadhiwa na kutunzwa katika hali ya usafi na usalama.

ii. Mwanachuo anayeharibu au kupoteza mali ya chuo atalazimika kufidia kwa kulipa kifaa chenyewe au kulipa fedha inayolingana na gharama ya kifaa hicho. Adhabu yake ni kutopewa vyeti vyake vyote hadi atakapolipia gharama ya uharibifu.

iii. Ni jukumu la kila mwanachuo kuripoti mara moja kila anapoona kitu ambacho si cha kawaida ambacho ni kinyume na taratibu za chuo au kuona mtu wa nje ambaye anamshuku kuwa ameingia isivyo halali. Hii inahusu pia kutoa taarifa kwa Uongozi wa chuo juu ya uwepo wa Mwanachuo aliyefukuzwa au kusimamishwa chuo au mafunzo.

iv. Ni wajibu wa kila mwanachuo kulinda na kutunza vema mali yake. Uongozi wa chuo hautahusika na upotevu wa mali yoyote ya mwanachuo.

11. KENGELE MAALUMU (ALARM BELL)

Hii ni kengele itakayogongwa muda wowote usio wa kawaida. Kila mwanachuo asikiapo mlio wa kengele hiyo aripoti haraka sana mahali anapotakiwa kufika hata kama anaumwa. Ni kosa kubwa kuchelewa au kupuuza wito wa namna hiyo.

12. SAA YA KULALA:

Muda wa kujisomea usiku (Preparation) utakoma saa 5:00 usiku. Kila mwanachuo anatakiwa kuwa chumbani pake ifikapo saa 5:20 usiku kwa kulala na ifikapo saa 5:30 usiku, taa zote zizimwe, redio zote zifungwe. Muda wa ziada wa kujisomea utatolewa kwa kibali maalumu.

13. MAVAZI:

Kila mwanachuo atatakiwa kuvaa sare ya chuo na kitambulisho wakati wote wa vipindi na awapo nje ya chuo kila siku.

Wasichana: Nguo ndefu zinazofunika magoti, zisizoonesha mwili (see through), zisizobana wala kuwa na mpasuo, na viatu visivyo na kisigino kirefu.

Wavulana: Suruali zenye marinda na zisizobana. Hakuna mwanachuo atakayeruhusiwa kuvaa kofia, Kanzu, kandambili, viatu vyenye kisigino kirefu au kaptura katika mazingira ya

chuo wakati wa vipindi na wakati mwingine wowote isipokuwa katika shughuli maalumu kama vile michezo, Bustani, shamba, au dini. Nje ya vipindi vya darasani mwanachuo anapaswa kuvaa nguo za heshima kama ilivyoelekezwa katika waraka wa mavazi kwa watumishi wa umma Na.3 wa mwaka 2007 na maboresho yake kwa kadiri itakavyoelekezwa na serikali. Nguo za michezo zivaliwe wakati wa michezo tu.

14. KAZI ZA MIKONO (KAZI INAENDELEA).

Kazi ni kipimo cha utu**,** uhai, msingi wa maisha bora na Elimu ya Kujitegemea ni sehemu ya mafunzo ya Ualimu. Kila mwanachuo atapaswa kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali ikiwa ni pamoja na kazi za shamba, bustani, utunzaji wa mazingira na mifugo ya chuo. Kushindwa kushiriki kikamilifu katika shughuli hizi ni sawa kabisa na kushindwa mafunzo ya Ualimu. Adhabu kali zitatolewa kwa atakaye kiuka sehemu hii ya mafunzo.

GERALD M RICHARD

MKUU WA CHUO

MKUU WA CHUO
CHUO CHA UALIMU
MPWAPWA

2021/2023

CHUO CHA UALIMU MPWAPWA

TAMKO LA AHADI YA KUFUATA KANUNI ZOTE ZA CHUO

"Soma kwa makini na kuelewa, kisha kiri kwa maandishi iwapo upo tayari kuishi kwa kufuata kanuni za chuo".

AHADI

Nakiri kuwa nimesoma na kuelewa kanuni zote za chuo, na kwamba ili niwe mfano mzuri kwa tabia na matendo yangu kwa wanachuo wenzangu na jumuiya yote ya chuo, naahidi kufuata kanuni zote na kwamba nikikiuka kanuni hizo nipo tayari kuwajibishwa kwa mujibu wa kanuni za chuo.

Naahidi kwamba nitafuata maelekezo na kutii viongozi wa serikali ya Wanachuo,Wakufunzi, na Wafanyakazi wa chuo wakati wote wa Mafunzo yangu.

Jina la Mwanachuo----------

Sahihi----------

Masomo ----------

Tarehe----------

GERALD M RICHARD

MKUU WA CHUO

MKUU WA CHUO
CHUO CHA UALIMU
MPWAPWA

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

2022-2023